JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS - IKULU

# Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania, (MKURABITA)

## Warsha ya Pili ya Walengwa wa MKURABITA Itakayofanyika tarehe 15.0202006 Jengo la NSSF- Waterfront, Dar es Salaam.

## Mada Kuhusu Utayarishaji wa Maboresho na Hatua za Baadaye

**Imetolewa na**

**Menejimenti ya MKURABITA**

**15.02.2006**

15 Februari, 2006

# UTANGULIZI

- Utayarishaji wa maboresho ni hatua ya pili katika awamu nne za Mpango huu.
- Mapendekezo ya maboresho yanatokana na matokeo yaliyojiri katika ripoti ya tathmini ya sekta isiyo rasmi;
- Sheria, kanuni na taratibu zilizopo za umiliki mali na kufanya biashara ni ngumu, zina gharama kubwa na urasimu.
- Kuna mifumo inayoongoza mahusiano na matendo ya jamii zilizo katika sekta isiyo rasmi na imeanishwa katika mila zao.
- Kanuni na taratibu hizi zina ubora wa kutosha kuwa msingi au mbegu ya maboresho yanayokusudiwa.

# UTANGULIZI

**Lengo la Maboresho ni;**

- Kukidhi azma ya kurasimisha rasilimali na biashara za wanyonge.
- Kuimarisha utawala wa sheria.
- Kukuza uchumi na kupunguza umaskini ni lazima yawe shirikishi yakilenga kuwawezesha walengwa kisheria na kiuchumi.


# UTANGULIZI

**Mchakato wa utayarishaji maboresho utajikita katika;**

- kuziboresha kanuni na miundo ya kitaasisi itumikayo sasa katika sekta isiyo rasmi.
- Kuboresha sheria za sasa za umiliki mali na uendeshaji biashara.
- Kuziunganisha ili kuwa na mfumo mmoja wa kitaifa wa sheria za umiliki mali na uendeshaji wa biashara.

# SURA YA MCHAKATO WA KUANDAA MABORESHO

## Miundo ya Sheria: Badiliko toka Juu kwenda Chini.




**Miundo ya Sekta Isiyo Rasmi: Badiliko toka Chini kwenda Juu.**

# MADHUMUNI YA MABORESHO

**Madhumuni ya Msingi ya Maboresho**.

- Kuandaa mapendekezo na mabadiliko yanayohitajika kisera na kitaasisi.
- Kuandaa mkakati wa utekelezaji wa mabadiliko yanayokusudiwa.
- Kurasimisha sekta isiyo rasmi ili iweze kushiriki katika shughuli za uchumi kwa mujibu wa sheria na hatimaye kuweza kuchangia katika ukuaji wa pato la Taifa kwa ufanisi zaidi na kupunguza umaskini wa kipato kwa wahusika/Walengwa

# UTAYARISHAJI WA MABORESHO

**Utayarishaji wa maboresho utalenga katika mambo yafuatayo;**

- Kuziunganisha na kuziboresha kanuni na taratibu zinazotumiwa sasa na wamiliki mali na wafanyabiashara katika sekta isiyo rasmi ili ziweze kuwa sehemu ya mfumo mpya wa sheria za umiliki mali na kufanya biashara.
- Kuzichunguza sheria za sasa zinazotumika kumiliki mali na kufanya biashara katika sekta rasmi ili kuzirekebisha ziweze kuoanishwa na kanuni na taratibu zilizotajwa hapo juu, katika kuandaa mfumo mpya wa sheria za umiliki mali na uendeshaji wa biashara.

# UTAYARISHAJI WA MABORESHO

- Kupendekeza mfumo wa utekelezaji, taasisi husika na kugawa majukumu.
- Kuandaa mkakati wa elimu, habari na mawasiliano ili kuwa na mfumo wa ushirikishwaji wa wadau.
- Kukadiria gharama za utekelezaji wa maboresho na kuandaa mkakati wa kuyagharamia ikiwa ni pamoja na kutafuta fedha.
- Kupunguza gharama za kumiliki mali na kufanya biashara ndani ya soko rasmi.

# UTAYARISHAJI WA MABORESHO

- Kuandaa kampeni kabambe ya urasimishaji mali na biashara itakayozingatia maboresho yaliyofanywa
- Kuwezesha walengwa kutumia mali walizonazo kujipatia mtaji, kuongeza tija na kuimarisha mgawanyo wa majukumu kwa ufanisi zaidi.
- Kuandaa utaratibu utaokaowezesha MKURABITA kuratibu na kushiriki katika shughuli maalumu za urasimishaji kama vile utengenezaji wa vitambulisho vya uraia, uanzishaji na uendelezaji wa masijala za ardhi na biashara n.k.

# UTAYARISHAJI WA MABORESHO

Kutokana na hadidu za rejea za mpango wa kazi, utayarishaji wa maboresho umepangwa kuanza rasmi hapa nchini mwezi Februari, 2006. Utekelezaji wa mpango wa kazi wa utayarishaji wa maboresho unakusudiwa kuchukua miezi 22.

# UHUSIANO KATI YA MKURABITA NA MABORESHO YANAYOENDELEA

Maboresho katika sekta za kiuchumi na kijamii yanayo endelea nchini Tanzania, yanajikita katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania **(MKUKUTA).**

Baadhi ya maboresho hayo ni;

- Maboresho katika Utumishi wa Umma.
- Maboresho katika Huduma za Kifedha.
- Maboresho katika Serikali za Mitaa
- Maboresho yanayohusu Mazingira ya Biashara
- Maboresho katika Sheria n.k

# UHUSIANO KATI YA MKURABITA NA MABORESHO YANAYOENDELEA

Utayarishaji wa maboresho yaliyokusudiwa yatatambua kuwepo na maboresho yaliyotajwa awali ili kuweza kuoanisha shughuli za urasimishaji na vipengele mahsusi vya MKUKUTA vinavyohusu upunguzaji umaskini wa kipato kwa njia ya kupanua ajira, uzalishaji na biashara.

# HATUA ZA BAADAYE UTEKELEZAJI WA MABORESHO

**Hatua za baadaye ni:**

- Utekelezaji wa Maboresho
- Ukuzaji wa Mitaji na Uimarishaji wa Utawala Bora.

**Utekelezaji wa Maboresho.**

- Kuunda taasisi maalumu yenye mamlaka ya kisheria sambamba na uandaaji wa maboresho.
- Taasisi hii itategemewa kuongoza utekelezaji wa maboresho yaliyoandaliwa kupitia Mpango huu na kuratibu shughuli zote za urasimishaji nchini.

# HATUA ZA BAADAYE UTEKELEZAJI WA MABORESHO

Taasisi itafanya kazi kwa kutumia mfumo ulioko wa Serikali za Mitaa, Wizara na Taasisi nyingine husika;

- Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi
- Wizara ya Usalama wa Raia
- Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko
- Wizara ya Sheria na Katiba

- Mpango kabambe wa urasimishaji utaanza baada ya kupitishwa sheria mpya itayoweka mfumo mpya wa kumiliki mali na kufanya biashara.

# HATUA ZA BAADAYE UTEKELEZAJI WA MABORESHO

**Mfumo Mpya Unakusudiwa Kuboresha;**

- Upimaji na upatikanaji wa ardhi kwa makazi na shughuli za maendeleo kwa haraka na kwa bei nafuu kuliko iliyo sasa.

- Utoaji wa hati miliki za ardhi kwa haraka na kulingana na mahitaji.

- Uandaaji na uwekaji wa mawasiliano kutoka vijijini hadi mijini, yatakayowezesha kuratibu mwenendo mzima wa urasimishaji wa rasilimali na biashara.

- Uandaaji na utekelezaji wa mpango wa kujenga uwezo wa walengwa ili waweze kutumia rasilimali zao zilizorasimishwa kujipatia mitaji na kuongeza ufanisi katika shughuli zao.

- Uandaaji wa utaratibu mpya wa kudhamini mikopo kutoka kwenye mabenki na vyombo vingine vya fedha kwenda kwa walengwa utakaozingatia;

✓ Uwezekano wa kutumia vyama au makundi maalumu kukopa kwa niaba ya wanachama.

✓ Kutumia mifuko maalum ya fedha kama dhamana ya ziada na kinga dhidi ya kufilisiwa mkopaji mdogo.

# HATUA ZA BAADAYE

Utaratibu huu utazingatia maslahi ya mkopeshaji bila kuvuruga umuhimu wa umiliki mali na kufanya biashara kwa mkopaji.

- Uandaaji wa miongozo rahisi ya kuanzisha biashara au kampuni, kuendeleza na hata kuzifunga bila kuathiri mali binafsi za mmiliki.

# HATUA ZA BAADAYE
# UKUZAJI WA MITAJI NA UIMARISHAJI WA UTAWALA BORA

**Ukuzaji wa Mitaji na Uimarishaji wa Utawala Bora.**

Mfumo mmoja wa kisheria wa umiliki mali unafungua milango kwa wale wote walioko katika sekta isiyo rasmi waweze kuingia katika mfumo rasmi unaotawaliwa na sheria;-

- Utaratibu mahsusi utaandaliwa ili wale wote waliorasimisha rasilimali zao waweze kufaidika na fursa za
  - ✓ Mikopo
  - ✓ Uwekezaji
  - ✓ Elimu
  - ✓ Sehemu za kudumu za kufanyia biashara.

# HATUA ZA BAADAYE

## Ukuzaji wa Mitaji na Uimarishaji wa Utawala Bora

- Uhusiano madhubuti kati ya wamiliki mali na wafanyabiashara na vyombo vya fedha, uchumi, masoko elimu ya biashara utaanzishwa katika awamu hii.
- Uwezeshaji wa mamlaka mbalimbali katika jamii hasa Halmashauri za Wilaya na Manispaa kuwa na mchakato wake wa urasimishaji; kwa kuwa mazingira, uwezo na kasi za jamii zetu mbalimbali zinatofautiana katika mchakato mzima wa urasimishaji.
- Kuongezeka kwa uwajibikaji kwa walengwa wetu kwa kuwa rasimali na biashara zilizorasimishwa zitatambuliwa au kufanywa kwa mujibu wa sheria, hivyo mapato na matumizi yake yatakuwa bayana.

# HATUA ZA BAADAYE
## Ukuzaji wa Mitaji na Uimarishaji wa Utawala Bora

- Kodi na ada zingine zitalipwa kwa mujibu wa sheria na walengwa watapata kinga ya kisheria dhidi ya athari za kufilisikia kwa biashara.

# CHANGAMOTO

- Matokeo ya utafiti katika sekta isiyo rasmi yameamsha ari kubwa kutoka kwa walengwa na wadau wengine kutaka kuona utekelezaji wa mpango huu mapema iwezekanavyo.
- Kuwezesha wananchi ambao wana hamu ya kuanza kurasimisha rasilimali na biashara zao sasa hata kabla ya maboresho hayajakamilika na kuanza kutelezwa.
- Kuelimisha walengwa na wadau wengi dhana na mchakato mzima wa mpango huu bila kufifisha matumaini yao ya kufanikiwa kwa kupitia mpango huu. (Hati ya umiliki mali pekee si kigezo tosha cha kupata mkopo au kuongeza mapato).

# CHANGAMOTO

- Taratibu za kuwashirikisha wadau katika uandaaji wa maboresho na kujenga uwezo wao katika kumiliki na kutekeleza awamu zijazo za Mpango, ni nyezo kuu katika kuimarisha ari za walengwa kutoka walipo na kuingia katika mfumo rasmi.

- Ushirikishwaji wa walengwa katika Mpango walioko maeneo ya vijijini.

# MUHIMU

- MKURABITA ni mpango mkubwa unaoashiria mabadiliko ya kimsingi katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini. Mafanikio yake yatategemea ushirikino mpana ndani ya Serikali, Sekta binafsi, Vyama vya Kiraia, wanasiasa na hata nje ya nchi.

- Mpango huu si juhudi za kuimarisha sekta isiyo rasmi, bali ni juhudi za kupunguza ukubwa wa sekta hiyo katika uchumi na kuimarisha sekta rasmi.

- Mafanikio ya mpango huu yataonekena pale wanyonge watakapoweza kuingia ama kutoka katika soko huria la kisasa kwa mlango ule ule unaotumiwa na wenye uwezo kwa mujibu wa sheria na kanuni zitumiwazo na wote ili kufaidi fursa zilizopo.

# ASANTENI KWA KUNISIKILIZA